TANGAZO LA SERIKALI NA. 216 la tarehe 28/3/2025

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA,
(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya vifungu vya 7(1) na 16(1))*

SHERIA NDOGO YA MAREKEBISHO YA SHERIA NDOGO YA ADA NA USHURU YA HALMASHAURI YA WILAYA YA SIMANJIRO YA MWAKA 2025

Jina

TS. Na. 510 la 2024

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Marekebisho ya Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro ya Mwaka 2025, na itasomwa pamoja na Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro ya Mwaka 2024 ambayo katika Sheria Ndogo hii inarejewa kama "Sheria Ndogo kuu".

Marekebisho ya kanuni ya 6

2. Sheria Ndogo kuu inarekebishwa katika kanuni ya 6 kwa-

(a) kufuta kanuni ndogo ya (1) na kuiandika upya kama ifuatavyo:

"(1) Halmashauri itahakikishwa kwamba ada au ushuru unakusanywa wakati wote katika maeneo yake.";

(b) kufuta kanuni ndogo ya (2); na

(c) kubadili mpangilio wa kanuni ndogo za (2) na (4) kuwa kanuni ndogo za (2) na (3) mtawalia.

Marekebisho ya Jedwali la Kwanza

3. Sheria Ndogo kuu inarekebishwa katika Jedwali la Kwanza-

(a) katika Sehemu ya Kwanza, kwa kuongeza maneno "shughuli mbalimbali" mara baada ya maneno "kwa ajili ya" yaliyopo katika safu ya pili ya kipengele cha 2;

(b) katika kichwa cha habari cha Sehemu ya Tatu

kwa kuweka maneno "ADA AU" kabla ya neno "USHURU";

(c) katika Sehemu ya Tatu, kwa kuondoa maneno "(Tani 1000)" yaliyopo katika safu ya nne ya kipengele cha 1;

(d) katika Sehemu ya Tano, kwa kufuta na kuandika upya vipengele vya 1 na 2 kama ifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| "1. | Jengo la makazi | 50,000/= | kwa kibali |
| 2 | Jengo la makazi ghorofa moja | 70,000/= | kwa kibali."; |

(e) katika Sehemu ya Sita, kwa kufuta kipengele cha 1;

(f) katika Sehemu ya Kumi na Moja, kwa kufuta maneno "Inategemea na Zao linalovunwa" yaliyopo katika safu ya pili ya kipengele cha 2 na badala yake kuweka maneno "shilingi 300,000/= kwa mwaka";

(g) katika Sehemu ya Kumi na Mbili (b) kinachohusu Ada ya Mashamba Makubwa, kwa kufuta tarakimu "500,00=" iliyopo kwenye safu ya tatu ya vipengele vya 1 na 2 na badala yake kuweka tarakimu "500/="; na

(h) kwa kubadili mpangilio wa Sehemu ya Nane hadi Sehemu ya Kumi na Mbili kuwa Sehemu ya Saba hadi Sehemu ya Kumi na Moja mtawalia.

Dodoma,
10 Januri, 2025

MOHAMED OMARY MCHENGERWA,
*Waziri wa Nchi-OR-TAMISEMI*